

HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA IDARA YA MAJI

Sekta ya maji ina lenga kufikisha huduma ya maji katika maeneo yote ya pembezoni mwa mji hususani katika maeneo ya Kata za Kishiri, Lwanhima na Luchebele pia kuhakikisha kuwa maeneo yote ya utoaji huduma za kijamii kama Zahanati, Hospitali ya Wilaya, Vituo vya Afya, Shule za Msingi na Shule za Sekondari zinapata huduma za Maji endelevu.

Mpaka sasa Idara imefikisha huduma ya maji katika maeneo ya Fumagila, Luchebele ziwani na Kilimo kishili kupitia Mfuko wa Maji vijijini na pia inaendelea na ujenzi wa mradi wa usambazaji maji katika kata ya Lwanhima.

Aidha, katika sekta hii inatoa elimu ya usimamizi wa miradi ya maji kwa vikundi vya watumiaji wa maji (COWSO) na wasimamizi wa magati ya maji pale mradi unapokamilika.

Hata hivyo huduma ya maji safi na salama kwa baadhi ya taasisi za serikali imekamilika, mpaka sasa shule za msingi zenye huduma ya maji ni 70, shule za sekondari zenye huduma ya maji ni 27, zahanati zenye huduma ya maji ni 12 na vituo vya afya vyenye huduma ya maji ni 2.

Huduma ya Maji safi na Salama katika maeneo ya pembezoni mwa mji imeongezeka kutoka asilimia 42 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 60.9 mwaka 2017 na tumefanikiwa kuongeza idadi ya vituo vya kuchotea maji kutoka 29 hadi 81 kwa maeneo ya Luchebele ziwani, Kishili kilimo na Fumagila kwa jumla ya miradi ya maji iliyokamilika.

Hata hivyo Idara ina majukumu ya kulida, kusimamia na kukagua miradi yote ya maji iliyokamilika na inayoendelea kutekelezwa chini ya Halmashauri ya Jiji kwa kuzingatia michoro inavyoelekeza ili kuhakikisha huduma ya maji inafika kwa wananchi kama ilivyopangwa na kuwa endelevu.

Naomba kuwasilisha,

Eng Zubeda Saidi

K N Y. MKURUGENZI WA JIJI